



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA

**MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA
MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI [THE WRITTEN LAWS
(MISCELLANEOUS AMENDMENT) (No.2) ACT OF 2016]**

Juni, 2016

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA
KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO
YA SHERIA MBALIMBALI [THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS
AMENDMENT) (No.2) ACT OF 2016]**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 ya Mwaka 2016 [The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.2) Act Of 2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana kwa mara ya kwanza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, katika Ofisi za Bunge, Dodoma mnamo tarehe 08 Juni, 2016 ili kupokea maelezo kuhusu Muswada husika.

Katika maelezo yake, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alieleza Kamati kuwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali [The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.2) Act Of 2016 unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Ishirini na Moja (21) kwa lengo la kuondoa mapungufu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo; kuongeza masharti mbalimbali ili kuleta uwiano kati ya Sheria hizo na Sheria nyingine na kurahisisha; kufuta baadhi ya vifungu

ambavyo vinaleta mkanganyiko katika utekelezaji wa Sheria husika au vimepitwa na wakati; na kuweka masharti mapya kwa ajili ya utekelezaji madhubuti wa Sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho.

Baadhi ya mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu, ni kubadilisha vifungu vya Sheria kwa kuondoa baadhi ya vifungu vya Sheria na kuingiza vifungu vipyta, kufuta baadhi ya Maneno, kuingiza maneno au tafsiri mpya na kuongeza vipengele vipyta. Mapendeleko yanayokusudiwa na Muswada huu yanalenga kukidhi matumizi ya sheria yaliyojitokeza na kuwezesha utekelezaji bora wa Sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho.

Mhesimiwa Spika, Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa ni kama zifuatazo:-

- a) Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423, (*The Anti-Money Laundering Act, Cap.423*).
- b) Sheria ya Kudhibiti Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432, (*The Anti-Trafficking in Persons Act, Cap.432*).

- c) Sheria ya Kanuni za Madai, Sura ya 33, (*The Civil Procedure Code, Cap.33*).
- d) Sheria ya Usajili wa Makandarasi, Sura ya 235, (*The Contractors Registration Act, Cap.235*).
- e) Sheria ya Elimu, Sura ya 353, (*The Education Act, Cap.353*).
- f) Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366, (*The Employment and Labour Relations Act, Cap.366*).
- g) Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6, (*The Evidence Act, Cap.6*).
- h) Sheria ya Taasisi za Kazi, Sura ya 300, (*The Labour Institutions Act, Cap.300*).
- i) Sheria ya Misitu, Sura ya 323, (*The Forests Act, Cap 323*).
- j) Sheria ya Uhamiajji, Sura ya 54, (*The Immigration Act, Cap. 54*).
- k) Sheria ya Mtoto, Sura ya 13, (*The Law of the Child Act, Cap.13*).

- l) Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216, (*The Land Disputes Courts Act, Cap.216*).
- m) Sheria ya Afya ya Akili, Sura ya 98, (*The Mental Health Act, Cap.98*).
- n) Sheria ya Baraza la Kiswahili Tanzania, Sura ya 52, (*The National Kiswahili Council Act, Cap.52*).
- o) Sheria ya Makamishna wa Viapo, Sura ya 12, (*The Notaries Public and Commissioners for Oaths Act, Cap. 12*).
- p) Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16, (*The Penal Code, Cap.16*).
- q) Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19, (*The Prevention of Terrorism Act, Cap.19*).
- r) Sheria ya Kusimamia Mirathi, Sura ya 352, (*The Probate and Administration of Estates Act, Cap. 352*).
- s) Sheria ya Madaktari wa Mifugo, Sura ya 319, (*The Veterinary Act, Cap.319*).
- t) Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, Sura ya 283, (*The Wildlife Conservation Act, Cap. 283*).

u) Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398, (*The Public Leadership Code of Ethics Act, 398*).

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ilitoa mwaliko na matangazo katika Vyombo vya Habari ili kuwaalika Wadau mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 ili kutoa maoni yao kuhusu vifungu mbalimbali vinavyokusudiwa kurekebishwa kwenye Sheria nilizozitaja kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

Aidha, baadhi ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge ambazo marekebisho ya Sheria hizo yalikuwa yanagusa Wizara na Taasisi za Serikali ambazo Kamati zao zinaisimamia na kuishauri Serikali, walihudhuria vikao vya Kamati na kutoa maoni ya Kamati zao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wadau wote ambao, kwa nyakati tofauti, waliwasilisha maoni yao mbele ya Kamati. Wadau hao ni Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufaa, Sekretarieti ya Msaada wa Kisheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Health Promotion Tanzania na Chama

cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC). Kamati ilipokea na kufanya kazi maoni ya Wadau hao, ambayo yameisaidia Kamati kwa kiasi kikubwa kuweza kuboresha Muswada huu.

2.0 MAONI YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu, naomba sasa niwasilishe Maoni ya Kamati ambayo yametokana na uchambuzi wa Wajumbe wa Kamati katika Sehemu na Ibara mbalimbali za Muswada.

SEHEMU YA PILI YA MUSWADA

Marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu (The Anti- Money Laundering Act), Sura ya 423

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4 ya Muswada wa Sheria hii inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 13 (a) cha Sheria Mama kinachoweka masharti kuhusu adhabu ya kosa la kutakatisha fedha haramu linalotajwa kwenye Kifungu cha 12. Kwa mujibu wa kifungu hiki adhabu inayotajwa ni faini ya kuanzia Shilingi Milioni Mia Moja (TZS. 100,000,000/=) hadi Shilingi Milioni Mia Tano (TZS. 500,000,000/=) au Kifungo cha kuanzia miaka mitano hadi miaka kumi (5 - 10) gerezani.

Marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza maneno “**or an amount equivalent to three times the market value of the property**,” mara baada ya maneno “**One Hundred Million Shillings**”.

Mabadiliko hayo yatakipanya Kifungu husika kisomeke kama ifuatavyo;

13. Any person who contravenes the provisions of Section 12 shall on conviction:

(a) If the person is an individual, be sentenced to a fine not exceeding Five Hundred Million Shillings and not less than One Hundred Million Shillings or an amount equivalent to three times the market value of the property, or to a term of imprisonment not exceeding ten years and not less than five years.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaafiki marekebisho yanayokusudiwa katika kifungu hiki kwani yataongeza adhabu kwa mtuhumiwa anayetiwa hatiani kwa makosa ya kutakatisha fedha haramu. Aidha, kuongeza adhabu huko kutasaidia mtuhumiwa kuadhibiwa kulingana na uzito wa kosa alilotenda, na hivyo kuondoa uwezekano wa kutakatishaji fedha zaidi ya kiwango kinachotajwa kwenye faini.

Ni wazi kuwa mapungufu yaliyopo katika kifungu cha sasa yanaweza kutoa mwanya kwa watu wanaojihusisha na

utakatishaji fedha haramu kutengeneza faida zaidi na kuzitumia kukwepa mkono wa sheria au kutumia sehemu ya mapato hayo haramu kulipa faini iliyopo kwa mujibu wa sheria pale wanapotiya hatiani. Tunapaswa kutoruhusu hilo kutendeka.

SEHEMU YA TATU YA MUSWADA

Marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti Usafirishaji Haramu wa Binadamu (*The Anti – Trafficking in Persons Act*), Sura ya 432.

Mheshimiwa Spika, katika Sehemu ya Tatu ya Muswada, Ibara ya 6 inakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti Usafirishaji Haramu wa Binadamu (*The Anti – Trafficking in Persons Act*) (Cap 432) kwa kukifuta na kukiandika upya Kifungu cha 14 (1) ambacho kinaweka masharti kuhusu kutaifisha mazalia ya uhalifu (Proceeds) na vifaa au mali zinazotokana na usafirishaji haramu wa binadamu. Kuandikwa upya kwa kifungu hiki kunalenga kuweka masharti kwa Mahakama, kuamua yenyele au kutokana na maombi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaweza kutoa amri ya kutaifisha mazalia na mali zote zilizopatikana kwa njia ya usafirishaji haramu wa binadamu pamoja na kitu chochote kilichotumika au kusaidia kosa la usafirishaji haramu wa binadamu kutendeka.

Kamati inakubaliana na pendekazo hilo kwa sababu Sheria ya sasa haina masharti yanayohusu kutaifisha kitu kilichotumika au kilichosaidia kosa hilo kutendeka, na pia haiweki masharti ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufungua maombi ya kuitaka Mahakama ifanye hivyo.

Vilevile, Ibara ya 7 ya Muswada huu inakusudia kukifanyia marekebisho Kifungu cha 20 (1) cha Sheria ya Kudhibiti Usafirishaji Haramu wa Binadamu (The Anti – Trafficking in Persons Act) (Cap 432) kwa kufuta maneno “task force” na badala yake kuweka maneno **“Anti – Trafficking Committee”**. Mabadiliko hayo yanalenga kuipa Kamati ya Kudhibiti Usafirishaji Haramu wa Binadamu ambayo imeanzishwa chini ya Sheria hii, jukumu la kuishauri Serikali pale inapoanzisha vituo vya ulinzi na msaada kwa Waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu. Kwa hali ilivyo sasa, jukumu hilo limewekwa chini ya Kikosi Kazi ambacho licha ya kutamkwa katika Sheria bado hakijaanzishwa na hivyo Serikali haina chombo cha kuishauri juu ya jambo hilo.

Kamati inakubaliana na mapendekazo hayo kwani biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu imekuwa ikiongezeka siku hadi siku ulimwenguni. Kwa kuzingatia ukweli kwamba, nchi yetu si kisiwa katika zama hizi za utandawazi, ni wazi, Waathirika wa biashara hiyo wanapaswa kupata ulinzi na

msaada wa uhakika pale wanapobainika ndani ya mipaka ya nchi yetu, na Serikali inaweza kutekeleza hilo kikamilifu kama itakuwa na chombo madhubuti cha kuishauri.

SEHEMU YA NNE YA MUSWADA

Marekebisho katika Sheria ya Mwenendo wa Madai (*The Civil Procedure Code*), Sura ya 33.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii lbara ya 9 ya Muswada inakusudia kukifanya marekebisho Kifungu cha 13 cha Sheria Mama kwa kukiwekea angalizo “provisor” linalotahadharisha kwamba, masharti yaliyopo katika kifungu hicho hayaondoi au kuchukua Mamlaka ya jumla ya Mahakama Kuu. Marekebisho yanalenga kuiwezesha Mahakama Kuu kutekeleza kikamilifu Mamlaka yake ya asili “*Inherent powers*” bila kufungwa au kubanwa na masharti ya kifungu hicho.

Kwa namna kifungu kilivyo sasa, kinaweka masharti kuwa kila shauri la madai litafunguliwa katika Mahakama ya ngazi ya chini yenyewe Mamlaka ya kusikiliza shauri husika na kwamba, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi ziko katika ngazi moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho yanayokusudiwa na Serikali katika Sheria hii hata

hivyo, inatahadharisha kwamba, Mahakama Kuu isije ikatumia angalizo hilo kuondoa mashauri ambayo yamewasilishwa katika Mahakama Kuu kwa sababu tu yalipaswa kusikilizwa na Mahakama za chini. Ni vyema kuwe na utaratibu wa kisheria ambao utaifanya Mahakama Kuu kuzingatia mazingira na umuhimu wa shauri husika, hivyo iwe na utaratibu wa kuhamisha mashauri ya aina hiyo yaliyowasilishwa kwake na kuyapeleka Mahakama husika.

SEHEMU YA TANO YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Makandarasi (*The Contractors Registration Act*), Sura ya 235

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya 5 ya Muswada kupitia Ibara ya 11 inakusudia kurekebisha Kifungu cha 6 cha Sheria Mama ambacho kinaweka masharti kuhusu uteuzi wa Msajili wa Makandarasi, kwa kukifuta na kukiandika upya na hivyo kukifanya kisomeke ifuatavyo:-

6 (1) The Board shall appoint a Registrar to the Board who shall be either a registered Engineer, Architect, Quantity Surveyor or a qualified person in either Law, Economics, Finance or Management.

(2) The Registrar shall hold or vacate Office in accordance with the terms of his appointment.

Kamati inaunga mkono pendekazo hili kwani linaongeza wigo wa kitaaluma kwa mtu anayeweza kuteuliwa kuwa Msajili wa Wakandarasi na kuondoa ukiritimba wa Sheria ya sasa ambayo inawataka watu waliosajiliwa kama Wahandisi na Wasanifu wa Majengo pekee ndiyo wawe na sifa za kuteuliwa katika nafasi ya Usajili.

Aidha, mapendekezo ya marekebisho katika kifungu hiki yamezingatia ukweli kwamba, kwa mujibu wa Sheria ya sasa utekelezaji wa majukumu ya Msajili siyo lazima yatekelezwe na watu wenye sifa zilizoainishwa.

Vilevile sehemu hii kupitia Ibara ya 12 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 10 kwa kuongeza kifungu kidogo kipycha (6) mara baada ya kifungu kidogo cha (5) ambacho kitasomeka ifuatavo:-

“(6) An applicant under this Section who is found guilty of an offence of submitting forged documents, misrepresentation or any form of fraudulent conduct, inducement or corrupt practice shall:

- (a) In the case of an applicant for registration as contractor**
 - (i) have his application deferred; and**
 - (ii) be debarred from being registered as contractor for a period of not more than two years; and**

- (b) in the case of an applicant for upgrading or for obtaining any service from the Board –**
- (i) have his application deferred;**
 - (ii) have his registration deleted; or**
 - (iii) be debarred as contractor for a period of not more than two years”**

Kamati inakubaliana na masharti ya hatua zinazokusudiwa na Bodi ya Usajili dhidi ya Makandarasi watakaobainika kudanganya, kugushi nyaraka au kujihusisha na vitendo vya rushwa wakati wa kuomba usajili au kupandishwa daraja, kwani yanalenga kuhakikisha kwamba Makandarasi wanaosajiliwa na bodi ni wale tu wenye sifa stahiki.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeshuhudia madhara mbalimbali yaliyotokana na uduni na kutozingatiwa kwa taaluma za kiuhandisi, ikiwa ni pamoja na kuperomoka kwa majengo ambayo yamejengwa chini ya viwango. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaona kuwa, kuongeza masharti ya adhabu dhidi ya ukiukwaji wa Sheria ya Usajili wa Wakandarasi, kutawafanya wahusika kuwa makini na kutekeleza majukumu yao kwa weledi na taaluma.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Ibara ya 13 ya Sehemu hii ya Muswada inakusudia kukifanyia marekebisho Kifungu cha 12

kwa kuongeza vifungu vipyta vidogo vya (2) na (3) mara baada ya Kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:-

"(2) An assessment of the majority shareholders shall be based on the aggregate of shares owned by locals in the individuals firm or company.

(3) Where the company applying for registration is a shareholder which is a limited liability company, the majority shareholding within that limited liability company shall be assessed to determine the aggregate shares owned between the locals and foreigners."

Maudhui ya marekebisho yanayokusudiwa katika kifungu hiki yanalenga kuboresha masharti ya vigezo vya Usajili wa Kampuni za Kigeni kwa kutaka tathmini ya kina ifanyike ili kubaini idadi ya hisa zinazomilikiwa na Wazawa katika kila Kampuni ua Ukandarasi.

Kamati inaafiki mapendekezo ya marekebisho yanayokusudiwa na Serikali katika kifungu hiki kwani yanalenga kudhibiti wimbi la Wageni kutumia Wazawa katika kusajili Kampuni na kushika kazi ambazo zingeweza kutekelezwa na Kampuni ya Kizawa pekee, na hivyo kujinufaisha zaidi kwa kigezo cha umiliki mkubwa wa hisa (*majority share holding*) ikilinganishwa na Wanahisa Watanzania katika Kampuni hizo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 14 katika sehemu hii ya Muswada inakusudia kukifanyia marekebisho Kifungu cha 13 cha Sheria Mama kwa kuongeza aya mpya ya (j) mara baada ya aya ya (i) ambayo itasomeka kama ifuatavyo:-

(j) Forgery, misrepresentation, fraudulent conduct, inducement or corrupt practice"

Kutokana na kuongezwa kwa aya hiyo mpya ya (i), sasa kutaifanya iliyokuwa aya (j) sasa kuwa aya (k) katika mtiririko wa aya za kifungu cha 13.

Ibara hii ya 14 inakifanyia marekebisho Kifungu cha 13 (6) kwa kukifuta na kukiandika upya kama ifuatavyo:-

"(6) A sole proprietor, partners, directors, or share holders of a company shall not be allowed to register a new contracting sole proprietorship or company after having been deleted as registered contractor for a period of three years unless otherwise directed by the Board"

Kamati inakubaliana na marekebisho yanayokusudiwa na Serikali kwani yanaweka masharti kuhusu kufuta Usajili wa Mkandarasi kwa kuongeza masharti kuwa Bodi inaweza kufuta jina la Mkandarasi katika Daftari la Makandarasi kwa makosa ya kughushi nyaraka, udanganyifu au vitendo vya rushwa, na kumzuia Mkandarasi huyo kuanzisha Kampuni nyingine hadi kipindi cha Miaka Mitatu kipite. Aidha, marekebisho haya

yatawafanya Wakandarasi kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria na miiko ya kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15 ya Muswada inakusudia kukifanyia marekebisho Kifungu cha 15(1) cha Sheria Mama kwa kuingiza maneno '**for a period to be specified by the Board**" mara baada ya neno "**suspend**". Marekebisho mengine yanalenga kufuta aya (c) kwa sababu masharti ya kumsimamisha Mkandarasi anayekiuka Kanuni au Sheria Ndogo zilizotungwa na Bodi, yanayotajwa katika aya hii tayari yameelezwa katika aya (a) na hivyo hakuna sababu ya kujirudia.

Vilevile sehemu hii inapendekeza kufutwa kwa aya (e) (ii), kwa sababu masharti ya kutaka Mkandarasi anayepata Leseni ya biashara bila kuwasilisha cheti cha Usajili kwenye Mamlaka inayotoa Leseni, afungiwe. Sababu ya mapendekezo hayo ni kutohana na ugumu unaojitokeza katika utekelezaji wa sharti hilo kwa sababu cheti cha usajili siyo mionganoni mwa vigezo vinavyozingatiwa na Mamlaka husika kabla ya kutoe Leseni.

Aidha, sehemu hii inapendekeza kuongezwa kwa Kifungu kidogo kipyaa cha (3) kitakachoweka masharti ya kumzuia Mkandarasi aliyesimamishwa kwa muda, kuendesha biashara, na pia kuipa Bodi Mamlaka ya kuamua kipindi ambacho Mkandarasi anaweza kusimamishwa asitekeleze shughuli za Ukandarasi.

Kamati inaafiki marekebisho haya kwa sababu yanalenga kuleta ufanisi katika shughuli za Ukandarasi, na kuwataka Wakandarasi wazingatie matakwa ya Sheria na miiko ya kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 16 ya Muswada inapendekeza kukifanyia marekebisho Kifungu cha 16 (1) cha Sheria Mama kinachotoa haki kwa Mkandarasi anayechunguzwa kwa ajili ya kusimamishwa, asikilizwe mbele ya Bodi. Marekebisho yanayopendekewa ni kuingiza maneno “**13 or**” mara baada ya maneno “**under section**”.

Kamati inakubaliana na marekebisho hayo kwa sababu yanalenga kuhakikisha, Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muunganio wa Tanzania, 1977 inayotoa haki ya kusikilizwa kikamilifu kwa mtu ambaye haki au wajibu wake vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa Mahakama au chombo kingine, inatekelezwa kikamilifu.

Ibara ya 17 ya Muswada inakusudia kukifanyia marekebisho Kifungu cha 17(1) cha Sheria Mama kinachozungumzia kudharau wito, amri au kukataa kutoa ushahidi wakati uchunguzi unafanywa na Bodi. Marekebisho yanayokusudiwa ni kuandika upya maneno ya utangulizi ya kifungu hicho ambapo sasa kitasomeka kama ifuatavyo:-

“Any contractor who, having been served with a summons under section 16(2)(b) or an order issued under the provisions of 16(2)(c), fails to comply or omits, without sufficient cause”

Kamati inakubaliana na marekebisho hayo kwa sababu yanalenga kufanya kifungu hicho kisomeke vizuri pamoja na kufanya rejea ya kifungu husika kinachoipa Bodi Mamlaka ya kutoa hati ya wito na amri wakati ikitekeleza majukumu yake ya kiuchunguzi chini ya Sheria hii.

Mhesimiwa Spika, marekebisho mengine yanayokusudiwa na sehemu hii ni yale yanayohusu Kifungu cha 23 (2) cha Sheria Usajili wa Makandarasi, ambapo inapendekezwa kufuta maneno “**within one year**” na badala yake kuweka maneno “**within sixty days**”

Mapendekezo hayo yana lengo la kupunguza muda ambao Kampuni ya Ukandarasi inaweza kufutwa na Bodi kwa kushindwa kupata Mkurugenzi Mtaalam baada ya Mkurugenzi ambaye ni Mwanahisa au Mbia kujuzulu, kutokuwa na uwezo (**Incapacitation**) au kufariki.

Kamati inaafiki mapendekezo hayo ya marekebisho kwani yatawezesha Kampuni za Ukandarasi kutokaa kipindi kirefu bila kuwa na Wataalam wenye sifa. Kipindi cha mwaka mmoja kinachotajwa kwenye Sheria ni kirefu sana na kinaweza kusababisha Kampuni ikapata kazi huku haina Wataalam

wanaokubalika kisheria na hivyo kazi hizo zikatekelezwa chini ya kiwango cha utaalam unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya mwisho kwenye sehemu hii ni katika Ibara ya 19 ambayo inakusudia kurekebisha Kifungu cha 33 cha Sheria Mama ambacho kinamtaka kila Mkandarasi kuandaa na kuwasilisha hesabu za mwaka (**Annual returns**) kwenye Bodi.

Marekebisho yanayopendekezwa ni kuyachukulia maudhui ya Kifungu cha 33 kuwa ni Kifungu kidogo cha (1) na kuongeza Kifungu kidogo cha (2) ambacho kitaweka masharti ya adhabu kwa atakayekiuka Kifungu kidogo cha (1). Kifungu kinachopendekezwa kitasomeka kama ifuatavyo:-

"(2) A person who contravenes subsection (1) commits an offence and is liable to a fine of 0.5% of the class limit."

Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo kwani yanalenga kuwafanya Wakandarasi wahakikishe wanaandaa na kuwasilisha hesabu zao kwenye Bodi kwa mujibu wa Sheria, na hiyo itaisaidia Serikali na Wadau kufahamu vyema uwezo wa kila Mkandarasi aliyesajiliwa.

SEHEMU YA SITA YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Elimu (*The Education Act*), Sura ya 353.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 21 ya Muswada huu inakusudia kufanya marekebisho katika Kifungu cha 60 (1)(k) kinachoweka masharti ya adhabu kwa mtu anayempatia ujauzito Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari au Msingi kuwa ni faini isiyozidi Shilingi Laki Tano na iwapo ni kosa la pili adhabu itakuwa ni faini ya Shilingi Laki Tano au kifungo kisichozidi Miaka Mitatu.

Marekebisho yanayokusudiwa na Muswada huu ni kukifuta kifungu hicho na kuandika kifungu kipyta cha 60A kitakachoweka masharti yanayo jitosheliza kuhusu zuio la kuoa au kumpa ujauzito Mwanafunzi wa Shule ya Msingi au Sekondari.

Kifungu kipyta kinachopendekezwa kinakusudia kuweka masharti ya kosa la jinai kwa:-

- (i) Mtu yeyote kuoa au kuolewa na Mwanafunzi wa Shule ya Msingi au Sekondari;
- (ii) Kijana wa Shule ya Msingi au Sekondari kuoa mtu yeyote; na

- (iii) Kwa mtu ye yote kumpatia ujauzito Mwanafunzi wa Shule ya Msingi au Sekondari.

Mheshimiwa Spika, adhabu inayopendekezwa kwa makosa hayo ni kifungo cha Miaka 30 gerezani. Aidha, Kifungu cha 60A kinapendekeza adhabu ya shilingi milioni Tano(5,000,000/=) au kifungo cha Miaka Mitano gerezani au vyote kwa pamoja kwa mtu atakayebainika kusaidia, kushawishi au kufanikisha Mwanafunzi wa Shule ya Msingi au Sekondari kuolewa au kuoa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona mantiki ya marekebisho yanayokusudiwa katika Sheria ya Elimu, kwamba yanalenga kumjengea Mwanafunzi wa Shule ya Msingi na Sekondari wigo wa ulinzi na mazingira mazuri ya kumwezesha akamilishe masomo yake kwa ngazi hizo. Hii ni pamoja na kutambua juhudzi za Serikali za kugharimia Elimu ya Msingi na Sekondari ili kutoa fursa ya Elimu kwa Watoto wote wa kitanzania. Hata hivyo, maoni ya Kamati ni kwamba, adhabu ya kifungo cha Miaka 30 inayotajwa katika mapendekezo iangaliwe upya ili kuondoa uwezekano wa Mtoto wa Kiume kutiwa hatiani na akajikuta akitabiliwa na adhabu hiyo, kukinzana na Sheria ya Mtoto ambayo inakataza Mtoto kufungwa gerezani, na pia kuonekana kama Majaji wanafungwa wasiweze kutumia utashi wao kutoa adhabu kwa wakosaji.

Ili kuzingatiwa kwa angalizo hilo, Kamati inashauri kutungwa kwa Kifungu kipyaa cha 60A (5) mara baada ya Kifungu cha 60A (4) ambacho kitasomeka ifuatavyo:-

"(5) Where the person convicted under subsection (2),(3) or (4) is a Child he shall be dealt with in accordance with the provisions of Section 119 of the Law of the Child Act"

Kamati inashauri kwamba ni vyema marekebisho yanayokusudiwa katika sehemu hii yakajumuisha makundi yote ya Watoto, hata wale wasio Wanafunzi kwani nao wanastahili kulindwa. Ili hilo liwezekane, ni vyema Vifungu 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa vikafanyiwa marekebisho kwa muktadha unaokusudiwa katika mabadiliko haya.

Mhesimiwa Spika, vilevile, Kamati inaona ni busara kwa marekebisho yanayokusudiwa katika sehemu hii kuzingatia mifumo mingine ya Elimu hasa ile ambayo Wanafunzi wake siyo Watoto kwa mujibu wa Sheria. Mfano ni Mpango wa Elimu Maalum kwa Walioikosa (MEMKWA) ambaao hutoa fursa kwa wale ambaao walikosa Elimu katika mfumo rasmi:- je, masharti haya ya Sheria nayo yatazingatiwa kwa Wanafunzi wa MEMKWA? Iwapo yatazingatiwa, haitakuwa kikwazo cha kuwakatisha tamaa Wanafunzi hao waliokosa Elimu katika mfumo rasmi?

SEHEMU YA SABA YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (**The Employment and Labour Relations Act**), Sura ya 366

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii, Ibara ya 24 inakusudia kufanya marekebisho katika Jedwali la Tatu katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini kwa kufuta maneno “by Labour Commissioner” yaliyopo katika aya ya 13 (5) na pia kufuta aya yote ya 13 (9).

Lengo la kufuta maneno yaliyotajwa katika aya ya 13 (5) ni kuipa uwezo Tume ya Usuluhishi na Uamuzi kusikiliza migogoro ya kikazi inayowasilishwa na upande wowote. Kwa Sheria ya sasa, migogoro inayotakiwa kufanyiwa kazi na Tume hiyo ni ile iliyowasilishwa na Kamishina wa Kazi tu.

Marekebisho ya aya ya 13 (9) yana lengo la kuondoa ukomo wa Miaka Mitatu unaowekwa katika kutumika kwa Ibara ya 13 ya Jedwali la Tatu la Sheria, na hivyo kutoa fursa kwa Watu kuwasilisha migogoro kwenye Tume hiyo kwa hatua muhimu ili isikilizwe na kuamuliwa kikamilifu.

Kamati inakubaliana na mapendekezo haya kwani yanalenga kuondoa vikwazo na ukiritimba na hivyo kuweka mazingira rahisi na rafiki kwa Wafanyakazi pale wanapowasilisha

migogoro kwenye Tume ya Usuluhihi na Uamuzi (CMA) kwa lengo la kufanyiwa kazi.

SEHEMU YA NANE YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Ushahidi (*The Evidence Act*), Sura ya 6.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 26 ya Muswada huu inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 127 cha Sheria ya Ushahidi, kwa kuongeza Kifungu kidogo kipya cha Nane (8) kitakachoweka masharti kuwa katika kesi za jinai ambayo ushahidi pekee ni wa mtoto, Mahakama inaweza kuupokea ushahidi huo baada ya kuridhishwa na ukweli (*Credibility*) hata kama haujaungwa mkono na ushahidi mwingine na ikamtia hatiani mshitakiwa.

Kanuni ya jumla katika uendeshaji wa kesi za jinai inataka ushahidi wa Mtoto mwenye Umri usiozidi Miaka 14 uungwe mkono na ushahidi mwingine ili uweze kuwa na nguvu kisheria.

Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali hasa kwa kuzingatia ukweli kwamba, masharti kama hayo tayari yanatumika katika kesi za jinai zinazohusiana na kujamiihana. Vilevile, marekebisho haya yataondoa uwezekano wa wahalifu kukwepa mkono wa Sheria kwa kigezo kwamba, ushahidi wa

Mtoto aliyeshuhudia tukio haukuungwa mkono. Hata hivyo, Kamati inatoa angalizo kwa Mahakama kuhakikisha inachukua juhudzi za makusudi za kujiridhisha kwamba, Mtoto husika anaeleza ukweli tupu, ili kuepuka uwezekano wa kutumia ushahidi ambao haujitoshelezi.

Aidha, Kamati inashauri kwamba, ni vyema utaratibu wa kusikiliza ushahidi wa Mtoto uzingatie mambo yaliyobainishwa kwenye shauri la Jinai la **Kimbute Otieno V. R CAT Cr. App 300/2011 at DSM.**

Kwa upande mwingine, Kamati ina maoni kwamba, ili marekebisho yanayokusudiwa yaweze kwenda vizuri ni vyema Vifungu vidogo vya (2) na (3) vikafutwa na badala yake kutunga Kifungu kipyaa kidogo cha (2) ambacho kitasomeka kama ifuatavyo:-

“(2) A Child of tender age may give evidence without taking an oath or making an affirmation but shall, before giving evidence, promise to tell the truth to the Court and not to tell any lies.”

SEHEMU YA TISA YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Misitu (*The Forests Act*), Sura ya 323

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 28 ya Muswada inapendekeza kufanyiwa marekebisho kwa Kifungu cha 88 cha Sheria ya Misitu ambacho kinaweka masharti ya adhabu kwa mtu anayekutwa na mazao ya misitu isivyo halali. Adhabu inayotolewa na kifungu hicho kwa sasa ni faini isiyozidi Shilingi Milioni Moja.

Marekebisho yanayopendekezwa katika Kifungu cha 88 yanakusudia kuongeza kiwango cha adhabu kwa kufuta maneno “**to a fine not exceeding One Million Shillings**” na badala yake kuweka maneno “**to a fine of not less than One Hundred Thousand Shillings but not exceeding Five Million Shillings**”.

Vilevile Ibara ya 29 ya Muswada katika sehemu hii inakusudia kukifanyia marekebisho Kifungu cha 89 cha Sheria ya Misitu kwa kufuta maneno “**to a fine of not less than Two Hundred Thousand Shillings and not exceeding One Million Shillings or to imprisonment for a term not exceeding two years**” yanayoonekana mwisho wa kifungu na badala yake kuweka maneno “**to a fine of One Million Shillings or Three times the market value of the prohibited produce whichever is greater or**

to imprisonment for a term not less than two years but not exceeding seven years",

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendelekezo yote katika vifungu vilivyotajwa hapo juu kwani yanalenga kuongeza adhabu kwa wote watakaokutwa na mazao ya misitu au kubainika kujihusisha na biashara ya mazao ya misitu isivyo halali. Ni jambo lisilopingika kwamba, kumekuwa na ongezeko la kasi ya uharibifu wa mazingira unaotokana na uvunaji haramu wa misitu. Kutookana na mantiki hiyo, ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali iangalie upya viwango vya adhabu vilivyowekwa ili viende sambamba na kiwango cha madhara ambayo yatatokana na uharibifu uliobainika kwa mkosaji.

SEHEMU YA KUMI YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji (*The Immigration Act*), Sura ya 54.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii lbara ya 31 inapendekeza marekebisho ya kuongeza Kifungu kipyaa cha 31A katika Sheria ya Uhamiaji. Kifungu hicho kipyaa kinalenga kuweka masharti kwamba, masuala ya usafirishaji wa Wahamiaji haramu ikiwemo kuhifadhi, kufadhili, kusafirisha, kusaidia usafirishaji wa Wahamiaji haramu ni kosa la jinai

ambalo adhabu yake ni faini isiyopungua Shilingi Milioni Ishirini au kifungo cha Miaka Ishirini gerezani.

Vilevile marekebisho katika kifungu hicho yanalenga kuiwezesha Mahakama kwa utashi wake au kutokana na maombi yatakayofunguliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, itoe amri kuwa mazalia au mali yoyote iliyopatikana kwa njia ya usafirishaji wa Wahamiaji haramu au kitu chochote kilichotumika kusaidia kosa hilo kufanyika, kitaifishwe na kuwa mali ya Serikali.

Kifungu hicho kipyä kitasomeka kama ifuatavyo:-

31A. A person who:-

- (a) *Smuggles immigrants;*
- (b) *Hosts immigrants;*
- (c) *Transports immigrants;*
- (d) *Finances, organizes or, aids the smuggling of immigrants;*
- (e) *Facilitates in anyway the smuggling of immigrants into the United Republic or to a foreign country;*
- (f) *Commits any fraudulent act or makes any false representation by conduct, statement or otherwise, for the purpose of entering into, remaining in or departing from, or facilitating or assisting the entrance*

into, reside in or departing from the United Republic of Tanzania,

commits an offence and on conviction, is liable to a fine of not less than twenty million shillings or imprisonment for a term of twenty years."

- (2) *In addition to the penalty imposed for the Commission of an offence under this Section, the Court may on its own motion or on the application by Attorney General, order confiscation and forfeiture to the Government of*
- (a) all proceeds and properties derived from the commission of the offence of smuggling immigrants; or*
 - (b) any thing used for purposes of committing or facilitating the commission of the offence of smuggling immigrants."*

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kuongeza adhabu kwa Watu wanaojihusisha na vitendo vya biashara ya Wahamiaji haramu kwani vitendo hivyo vimekuwa vikiongezeka siku hadi siku hapa nchini na kuhatarisha usalama na amani ya nchi yetu. Hata hivyo, ni maoni ya Kamati kwamba, marekebisho yanayokusudiwa yaweke masharti kwamba, adhabu itakayotolewa kwa mkosaji wa vitendo vya usafirishaji wa Wahamiaji haramu, itaendana na idadi ya Wahamiaji haramu ambao mhusika atabainika kuwasafirisha,

kuwahifadhi, au kuwasaidia. Kamati pia inashauri neon “*illegal immigrants*” litumike katika kifungu hiki badala ya neno “immigrants” ili kuondoa mkanganyiko wa maana au tafsiri ya neno hili linapotumika katika muktadha huu (*Ambiguity*)

SEHEMU YA KUMI NA MOJA YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Taasisi za Kazi (*The Labour Institutions Act*), Sura ya 300.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii, Ibara ya 33 inapendekeza marekebisho katika Sheria Mama kwa kuongeza Kifungu kipya cha 45A mara baada ya kifungu cha 45.

Kifungu hicho kipya kinakusaidia kuweka masharti yatakayompatia Afisa wa Kazi Mamlaka ya kutoza faini au tozo ya papo kwa papo kwa Mwajiri au Mtu ye yeyote anayekiuka masharti ya Sheria za Kazi ikiwa ni pamoja na kutowasilisha michango ya Wafanyakazi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Faini inayopendekezwa kutozwa chini ya kifungu hicho haitapungua Shilingi Laki Moja na Afisa wa Kazi atatoa risiti kwa kila malipo yanayofanywa.

Kamati inakubaliana na marekebisho yanayokusudiwa kwani, yanalenga kuhakikisha Waajiri wanazingatia kikamilifu masharti ya Sheria za Kazi na adhabu stahiki zinatolewa kwa wakosaji watakaokiri kosa, na hivyo kupunguza mashauri ya aina hiyo

kuchukua muda mrefu mahakamani. Baadhi ya Waajiri wamekuwa hawapeleki michango ya Waajiriwa wao kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, jambo ambalo limekuwa likidhoofisha utendaji wa mifuko hiyo, na pia kwa Wastaafu pale wanapofuatilia stahiki zao baada ya kustaafu.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Mtoto (*The Law of the Child Act*),

Sura ya 13.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Kumi na Mbili ya Muswada inahusu marekebisho yanayopendekezwa na Ibara ya 35 kwenye Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 (***The Law of the Child Act, Cap.13***) kwa kuongeza Kifungu kipyga cha 100A mara baada ya Kifungu cha 100.

Kifungu kinachopendekezwa kinalenga kuweka masharti kuhusu Mahakama kuzingatia maoni na mapendekezo ya Afisa Ustawi katika kesi inayomkabili Mtoto mbele ya Mahakama ya Watoto, iwapo itaona ni muhimu kufanya hivyo hasa wakati wa kutoa adhabu kwa Mtoto.

Kwa sasa, Sheria ya Mtoto inaelekeza juu ya Afisa Ustawi wa Jamii kuwepo wakati shauri linaendelea, hata hivyo Sheria haiweki bayana namna anavyoweza kuisadia Mahakama ya Watoto kufikia uamuzi wake.

Kamati inaunga mkono marekebisho haya kwani, sasa yatamuwezesha Afisa Ustawi wa Jamii, ambaye amekuwepo Mahakamani tangu shauri lilipofunguliwa, kuisaidia Mahakama ya Watoto kufikia uamuzi wa haki, na hasa kwa kuzingatia ukweli kwamba ana taaluma ya masuala ya Watoto.

Kifungu kinachopendekezwa kitasomeka ifuatavyo:-

100A. (1) *The Juvenile Court may, during the proceedings, where it considers necessary, seek the opinion and recommendation of Social Welfare Officer.*

(2) *Where the Court considers necessary to have the opinion or recommendation of a Social Welfare Officer, the Court shall consider such opinion or recommendation before the passing sentence.*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 36 ya Muswada inapendekeza kukifanyia marekebisho Kifungu cha 103 (1) cha Sheria ya Mtoto kwa kufuta maneno “Police Officer” na badala yake kuweka maneno “Public Prosecutor”.

Vilevile marekebisho yanapendekeza kufuta Kifungu kidogo cha (2) kinachoweka masharti kwamba, Mtoto anapofikishwa katika Mahakama ya Mtoto kwa kosa lolote isipokuwa kosa la mauaji basi kesi inayomhusu isikilizwe na imalizike siku hiyo hiyo. Kwa kuwa Mtoto anaweza kutenda makosa mengine ambayo yanatakiwa kufunguliwa katika Mahakama Kuu pekee,

marekebisho katika kifungu hiki yanalenga kuweka masharti kwamba, Mahakama ya Watoto haitasikiliza kosa linalotakiwa kusikilizwa na Mahakama Kuu ikiwemo kosa la mauaji linalotajwa kwenye Sheria ya sasa.

Aidha, inapendekezwa kwamba, iwapo usikilizwaji wa kesi iliyofunguliwa katika Mahakama ya Watoto hautamalizika siku hiyo hiyo kama inavyoelekezwa katika Kifungu cha 103 (2), basi Mahakama baada ya kuainisha sababu iahirishe kesi hiyo na imwachie Mtoto kwa dhamana.

Kamati inakubaliana na marekebisho haya kwani yanalenga kuiwezesha Mahakama ya Mtoto kushughulikia kesi ambayo haikuweza kumalizika ndani ya siku shauri husika lilipofunguliwa, kwani zipo sababu za msingi ambazo zinaweza kujitokeza kama vile ugonjwa kwa wahusika katika kesi, ushahidi au upelelezi kutokekamiliwa mapema.

Mhesimiwa Spika, marekebisho mengine katika Sehemu hii ni yale yanayopendekezwa na kifungu cha 37 ambacho kinakusudia kurekebisha Kifungu cha 119 kinachoweka masharti kuhusu zuijio la adhabu ya kifungo na adhabu mbadala kwa Mtoto (**Prohibition of custodial sentence and alternative sentence**).

Kifungu cha 119 (1) kinaelekeza kuwa Mtoto asihukumiwe kifungo gerezani, hata hivyo, Sheria za jinai zinaweka masharti

ya jumla kuwa Mtu anayetenda kosa la jinai anaweza kuhukumiwa kifungo gerezani bila kuelekeza kuwa masharti hayo hayatatumika kwa mshitakiwa Mtoto.

Mapendekezo ya Muswada yanakusudia kukiandika upya kifungu hicho ili kueleza kuwa masharti ya Mtoto kutoadhibiwa adhabu ya kifungo gerezani yatatumika bila kujali masharti ya Sheria nyingine za jinai. Vilevile, Muswada unapendekeza kuwa Mahakama ya Watoto inaweza kutoa adhabu ya viboko. Adhabu hiyo haipo kwenye Sheria ya sasa na inaonekana kuwa inaweza kusaidia kuwafanya Watoto waogope kutenda makosa ya jinai lakini pia inatambulika katika Sheria ya Kanuni za adhabu kuwa ni adhabu halali.

Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho yanayokusudiwa na Serikali kwani yanalenga kuwaepusha watoto kufungwa gerezani, ambako huwekwa pamoja na watu Wazima na hivyo baadhi ya haki zao kukiukwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu ya 39 ya Muswada inapendekeza kutunga Kifungu kipycha 158A katika Sheria ya Mtoto ambacho kinalenga kuzuia kukeketa Mtoto wa kike. Kifungu kidogo cha (2) kinaweka adhabu kwa kosa hilo kuwa ni faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili au kifungo kisichopungua Miaka Mitano (5) lakini kisichozidi Miaka Kumi na Mitano (15) au vyote kwa pamoja.

Kamati inaunga mkono marekebisho yanayokusudiwa pamoja na adhabu zake, kwani yanalenga kuzuia vitendo vya ukeketaji na kumlinda Mtoto wa kike dhidi ya madhara yanayotokana na vitendo hivyo.

SEHEMU YA KUMI NA TATU YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi (*The Land Dispute Courts Act*), Sura ya 216.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii Kifungu cha Muswada 41 kinapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 41 cha Sheria Mama kwa kuongeza kifungu kitakachoweka muda wa kukata rufaa dhidi ya maamuzi ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika Mahakama Kuu. Sheria ya sasa haina kifungu mahususi kinachoeleza muda wa kukata rufaa, na hilo limesababisha Mahakama Kuu kutoa maamuzi tofauti kuhusu jambo hili.

Kwa sasa upo mkanganyiko wa kisheria kuhusiana na muda wa kukata rufaa; wakati yapo maamuzi kwamba rufaa kutoka Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya inatakiwa kufunguliwa katika Mahakama Kuu ndani ya siku Arobaini na Tano(45) tangu uamuzi kutolewa, maamuzi mengine yanaeleza kwamba, muda wa kukata rufaa hiyo ni siku Tisini (90) kama

ilivyo katika Sheria ya Ukomo wa Muda, Sura ya 89 (*The Law of Limitation Act, Cap.89*).

Muswada unapendekeza kuweka sawa jambo hili kisheria kwa kurekebisha Kifungu cha 41 cha Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi na kuweka masharti kwamba muda wa kukata rufaa hiyo utakuwa siku Arobaini na Tano (45) tangu kutolewa kwa uamuzi na kwamba Mahakama inaweza kuongeza muda huo wa kukata rufaa baada ya kuridhika kuwa kuna sababu za kufanya hivyo. Sababu hizo zitaelezwa katika maombi yatakayofunguliwa na Mtu anayeomba kukata rufaa nje ya muda ulioainishwa katika Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwani yanalenga kuondoa utata uliokuwepo kuhusiana na muda wa kukata rufaa dhidi ya maamuzi ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

SEHEMU YA KUMI NA NNE YA MUSWADA

Marekebisheso ya Sheria ya Afya ya Akili (*The Mental Health Act*), Sura ya 98

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 43 katika sehemu ya Kumi na Nne ya Muswada, inapendekeza kufanya marekebisheso katika Jedwali la Pili kwa kuboresha Fomu Namba Tatu (3) inayohusu

amri ya kupokea (**Reception order**) Mtu katika Hospitali ya Afya ya Akili.

Marekebisho hayo yanakusudia kuweka sehemu ambayo Hakimu wa Wilaya au Hakimu Mkazi, atasaini fomu hiyo na kuweka muhuri wa Mahakama kabla ya kuiwasilisha kwa Afisa Mfawidhi wa Hospitali ya Afya ya Akili. Kwa namna Sheria ilivyo sasa, hakuna sehemu maalum kwa ajili ya Hakimu kusaini na kuweka muhuri wa Mahakama.

Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo ya Serikali kwani yanalenga kuwezesha kutambulikana kwa Hakimu aliyetoa amri ya kupokea (**Reception order**) Mtu katika Hospitali ya Afya ya Akili.

SEHEMU YA KUMI NA TANO YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Baraza la Kiswahili Tanzania (*The National Kiswahili Council Act*), Sura ya 52

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 45 ya Muswada huu inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Baraza la Kiswahili Tanzania, Sura ya 52, kwa kuongeza Kifungu kipyga cha 11 kitakachoweka masharti kumpa Waziri Mamlaka ya kutunga Kanuni. Kifungu hicho kipyga kitasomeka kama ifuatavyo:-

11. The Minister may make regulations in respect of any matter which under this Act is required or permitted to be prescribed

or is necessary or convenient for better carrying out or giving effect to this Act.”

Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kuhusiana na maarekebisho haya kwani Waziri atawezza kutunga Kanuni ambazo zitarahisisha utekelezaji bora wa Sheria hii, tofauti na ilivyo sasa katika Sheria ambapo hakuna masharti ya aina hiyo.

SEHEMU YA KUMI NA SITA YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Makamishina wa Viapo (*The Notaries Public and Commissioners for Oaths Act*), Sura ya 12

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 47 katika Sehemu ya Kumi na Sita ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 8 cha Sheria ya Makamishina wa Viapo, kwa lengo la kuweka masharti yatakayomtaka Kamishna wa Viapo kuweka jina lake katika kila kiapo anachoshuhudia.

Inapendekezwa kuingiza maneno “**insert his name and**” katikati ya maneno “**shall**” na “**state**” yaliyoko katika Kifungu hicho.

Kwa sasa, Kifungu hicho kinamtaka Kamishna wa Viapo kueleza mahali na tarehe ambayo kiapo husika kimetolewa, na hivyo halazimiki kuweka jina lake wakati wa kushuhudia kiapo.

Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwani, yanalenga kuwezesha Mahakama na Mamlaka nyingine kumfahamu Kamishna wa Kiapo aliyeshuhudia kiapo husika hususani inapotokea ubishani kuhusu uhalali wa kiapo hicho.

Vilevile, Kamati inaunga mkono wazo kwamba marekebiso yanayokusudiwa hayataathiri viapo ambavyo vilikwishatolewa na kuwasilishwa Mahakamani kabla ya marekebiso yanayokusudiwa kuanza kufanya kazi kwa mujibu wa Ibara ya 50 ya Muswada ambayo inaweka Kifungu kipyga cha 14 kuhusu mashari ya mpito.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 49 kinakusudia kurekebisha kifungu cha 13 cha Sheria hiyo kwa lengo la kumpa Jaji Mkuu Mamlaka ya kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti Sheria hii, tofuti na ilivyo sasa ambapo Mamlaka haya yako kwa Mahakama baada ya kupata kibali cha Rais. Marekebiso hayo yanaeleza kwamba, Mahakama Kuu kama moja ya Mahakama zilizopo itashirikishwa ipasavyo sambamba na Wadau wengine wakati wa kuandaa Kanuni hizo.

Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwani yanatambua Mahakama kama Muhimili na pia majukumu ya Jaji Mkuu kama Kiongozi Mkuu wa muhimili huo.

Marekebiso mengine katika Sehemu hii yanalenga kuongeza Kifungu kipyga cha 14 kinachompa Jaji Mkuu Mamlaka ya

kurekebisha Majedwali ya Sheria hiyo. Majedwali hayo yanahusu tozo kwa ajili ya nyaraka za kisheria, Fomu ya cheti cha kufanya kazi (**Practicing certificate**) na ada ya Vyeti vyaa Makamishna wa Viapo.

Marekebisheso hayo yanalenga kuweka utekelezaji bora wa Sheria hiyo kwa kuwezesha Majedwali hayo yarekebisheso na Jaji Mkuu pale kutakapokuwa na hitaji la kufanya hivyo bila kupeleka Bungeni marekebisheso hayo.

Mwisheso, Sehemu hii inapendekeza kurekebisha Jedwali la Tatoo kwa lengo la kuongeza viwango vyaa ada ya vyeti vinavyotolewa chini ya Sheria hiyo kama ifuatavyo:

- (a) Ada ya cheti cha kufanya kazi kama Kamishna wa Viapo iwe Shilingi Elfu Thelathini (Tshs. 30,000) badala ya Shilingi Sitini (Tsh. 60) inayotajwa kwenye Sheria sasa.
- (b) Tozo ya kulipia upya (**Renewal**) cheti kila mwaka iwe Shilingi Elfu Arobaini (Tshs. 40,000) badala ya Shilingi Arobaini (40) inayotajwa kwenye Sheria sasa.
- (c) Tozo ya maombi ya cheti kipyaa baada ya cheti kupotea au kuharibika iwe Shilingi Elfu Kumi (Tshs. 10,000) badala ya Shilingi Kumi (Tshs. 10) inayotajwa kwenye Sheria sasa.

Kamati inaafiki marekebisho yanayokusudiwa kwa sababu yanalenga kuweka viwango vinavyoendana na hali ya sasa kwani viwango vilivyopo kwenye Sheria vimepitwa na wakati na havikidhi haja.

SEHEMU YA KUMI NA SABA YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Kanuni za Adhabu (*The Penal Code*), Sura ya 16

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 53 ya Muswada huu inakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Kanuni za Adhabu, kwa kukifuta Kifungu cha 55 ambacho kinaoweka masharti kuhusu nia ya kuchochaea uasi (**Seditious intentions**).

Sababu ya kufuta kifungu hiki ni kwamba, masharti kuhusu nia ya kuchochaea usasi yaliyoko katika kifungu hicho yako pia katika Kifungu cha 31 cha Sheria ya Magazeti, Sura ya 229 (*The Newspapers Act, Cap. 229*). Aidha, kwa sasa Sheria ya Kanuni za Adhabu haina kosa la uchochezi kwani lilifutwa kupitia Kifungu cha 55 cha Sheria ya Magazeti, na kosa hilo liko katika Kifungu cha 32 cha Sheria ya Magazeti.

Kamati inaunga mkono mapendekezo haya ya Serikali kwani yanalenga kuwezesha kufanyika kwa rejea sahihi ya Sheria kuhusu nia ya kuchochea uasi.

SEHEMU YA KUMI NA NANE YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Ugaidi, (*The Prevention of Terrorism Act*), Sura ya 19

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 55 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti Ugaidi, kwa kuongeza kuongeza Kifungu kipyaa cha 11A kitakachoweka masharti kuhusu adhabu kwa makosa ya kuandaa, kusimamia, kuwezesha au kushiriki kwenye mikutano ya kigaidi, kuwezesha ugaidi, kuhifadhi magaidi kumiliki taarifa zilizozuiliwa na utoaji wa tishio la uongo la kigaidi yanayotajwa katika Vifungu vya 5,7 na 8 vya Sheria hiyo.

Kwa kuwa, Sheria ya Kuzuia Ugaidi ilivyo sasa haitaji adhabu kwa mtu anayetenda makosa ya ugaidi, Muswada unapendekeza adhabu kwa makosa hayo iwe, (i) kifo iwapo tukio la ugaidi limesababisha kifo, (ii) kifungo cha maisha iwapo kosa husika limesababisha madhara makubwa kwa mtu au mali na (iii) kifungo cha Miaka Thelathini kwa mazingira mengine.

Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwani licha ya kutoa mwongozo kuhusu adhabu inayostahili kutolewa kwa makosa ya ugaidi, yatadhibiti ipasavyo vitendo vya kigaidi ambavyo vimekuwa na athari kubwa kwa maisha ya watu na uchumi wa nchi kutokana na kuzorotesha amani.

Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia iwapo kweli adhabu ya kifo ina athari stahili kwa Wanaotiwa hatiani na Sheria kutokana na makosa ya vitendo vya kigaidi mantiki ya Kamati kuhoji hivyo ni kutokana na ukweli kwamba, adhabu hiyo inalengwa kutolewa kwa Watu amba wako tayari kujitoa uhai wao kutokana na vitendo wanavyovifanya. Ni maoni ya Kamati kwamba, kifungo cha maisha na kazi ngumu gerezani, au kifungo katika magereza maalum zingeweza kuwa adhabu muafaka.

SEHEMU YA KUMI NA TISA YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, (*The Probate and Administration of Estates Act*), Sura ya 352

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 57 ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 2 cha Sheria ya Usimamizi wa Mirathi, kwa kufuta tafsiri ya maneno “**small estate**” na badala yake kuweka tafsiri ifuatayo:-

“Small estate” means an estate the gross value of which a Court, District Court or other Authority having jurisdiction in probate or administration is satisfied, does not exceed One Hundred Million Shillings;”

Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuongeza ukomo wa kiwango cha thamani ya mirathi itakayoshughulikiwa na Mahakama ya Wilaya kutoka Shilingi Milioni Kumi kwenye Sheria ya sasa, hadi Shilingi Milioni Mia Moja, kwani yatawezesha Wananchi wengi kufungua mashauri ya mirathi yenye thamani ambayo haizidi Shilingi Milioni Moja katika Mahakama za Wilaya kutokana na ukaribu wa Mahakama hizo ikilinganishwa na Mahakama Kuu ambayo iko katika baadhi ya mikoa Tanzania Bara.

SEHEMU YA ISHIRINI YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Madaktari wa Mifugo, (*The Veterinary Act*), Sura ya 319

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii Kifungu cha 59 cha Muswada kinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 15 kwa kuongeza Kifungu kidogo cha (3) kitakachosomeka ifuatavyo:-

“(3) A person shall not be registered as a Veterinarian unless that person, in addition to the qualification stipulated under subsection (1), has undergone internship training for a period of not less than one year.”

Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwani, itaondoa uwezekano wa Mtu asiye na sifa kusajiliwa kuwa Daktari wa Mifugo. Aidha, marekebisho hayo yatasaidia kuboresha taaluma ya Udaktari wa Mifugo na kusisitiza juu ya viwango vinavyotakiwa kwenye usajili chini ya Sheria ya Madaktari wa Mifugo.

SEHEMU YA ISHIRINI NA MOJA YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, (*The Wildlife Conservation Act*), Sura ya 283

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 61 cha Muswada huu kinapendekeza kurekebisha Kifungu cha 86 kwa kuongeza Kifungu kidogo cha (2)(iii).

Kifungu hicho kinakusudia kuweka masharti ya adhabu ya faini isiyopungua mara tatu ya thamani ya soko ya nyara za Serikali au kifungo cha kuanzia Miaka Kumi hadi Miaka Ishirini gerezani kwa Mtu ambaye atakutwa na hatia kwa kosa la kumiliki nyara za Serikali kinyume na Sheria na thamani ya nyara hizo ikawa kati ya Shilingi Laki Moja hadi Shilingi Milioni Moja.

Kamati inakubaliana na mapendekezo haya ya Serikali kwani yanalenga kukabiliana na vitendo vya ujangili wa wanyamapor i kwa kuwaadhibu ipasavyo Watu wanaotiwa hatiani. Aidha, ni mtazamo wa Kamati kwamba, iwapo hatua za makusudi hazitachukuliwa dhidi ya majangiri, urithi wa Wanyamapor na maliasili uliopo utatoweza na vizazi vijavyo havitapata fursa ya kuushuhudia.

SEHEMU YA ISHIRINI NA MBILI YA MUSWADA

Marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, (*The Public Leadership Code of Ethics Act*), Sura ya 398

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Mbili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398.

Ibara ya 63 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 4 kwa kuongeza tafsiri ya maneno “**Child**” na “**Conflict of interest**” ili kuboresha utekelezaji bora wa Sheria hiyo kwa kuwa maneno hayo yametumika katika Sheria hiyo lakini hayajawekewa tafisri. Vilevile, marekebisho hayo yanalenga kumtaka kila Kiongozi wa Umma kuainisha maslahi yoyote katika kila jambo analolifanyia kazi au maamuzi.

Ibara ya 64 ya Muswada inapendekeza marekebisho kwenye Kifungu cha 6 cha Sheria Mama, ili kuongeza makatazo kwa

Kiongozi wa Umma na pia kutoa adhabu kwa Kiongozi yeyote wa Umma ambaye atakiuka maadili chini ya Sheria hii.

Makatazo hayo, yanajumuisha kutojihusisha na ajira binafsi inayohusiana na kazi aliyokuwa akiisimamia wakati akiwa katika Utumishi wa Umma hadi baada ya miezi sita tangu alipohitimisha utumishi wake, kutoshughulikia jambo ambalo ana maslahi nalo na kutoingia mkataba wowote na Serikali au chombo chochote cha Serikali yeye binafsi au familia au Kampuni yake.

Vilevile, Muswada unaongeza vifungu vipyta vya 18A na 18B ili kumpatia kinga Afisa wa Sekretarieti ya Maadili anayefanya kazi au kutekeleza majukumu kwa niaba ya Sekretarieti, ili asiwajibike yeye binafsi kwa jambo ambalo atalitenda kwa nia njema wakati akitekeleza wajibu wake. Sambamba na hilo, Muswada unapendekeza masharti ya adhabu ya faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja au kifungo kisichozidi mwaka mmoja gerezani au vyote kwa pamoja kwa mtu atakayemzuia Afisa wa Sekretarieti ya Maadili kufanya kazi zake.

Kamati inakubaliana na mapendekezo yanayokusudiwa na Serikali kwani yanalenga kuimarisha uzingatiwaji wa maadili kwa Viongozi wa Umma, hata hivyo haoni ni vipi kuo au kuolewa kwa mtoto wa kiongozi kunavyoweza kuwa na mantiki katika azma ya kurejesha au kuendeleza maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, Kamati inafikiri kuo au kuolewa hakuwezi

kuondoa sifa ya mtoto kupoteza sifa ya utoto kwa Wazazi wake, na baadhi ya viongozi wa Umma wanaweza kutumia mwanya huo kuficha mali ambazo hawakuzipata kihalali na wakafanikiwa kukwepa mkono wa sheria.

3.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kukushukuru kwa kutoa kibali ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi Muswada huu. Aidha, nawashukuru Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kisekta, ambao waliitikia mwaliko wa kutoa maoni kwa Sheria mbalimbali zinazohusu Sekta wanazozisimamia.

Nawashukuru Wataalamu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ambazo zinahusika na Sheria mbalimbali zinazopendekewa kurekebishwa kwa kutoa ufanuzi kwa Kamati katika maeneo mbalibali ya Muswada. Walifanya kazi hiyo kwa weledi na kujituma kwa lengo la kuhakikisha Muswada huu unachambuliwa vizuri kabla ya kuletwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na Wajumbe Waalikwa kwa weledi na umahiri wao

waliouonyesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekoz ya msingi ya kuuboresha.

Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (HANSARD)

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Dkt Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Seif Ungando Ally, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Ally Salehe, Mb – Mjumbe
10. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb – Mjumbe
11. Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb – Mjumbe
12. Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb – Mjumbe
13. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb – mjumbe
14. Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb – Mjumbe
15. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb – Mjumbe
16. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb – Mjumbe
17. Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb – Mjumbe
18. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb – Mjumbe
19. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb – Mjumbe
20. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb – Mjumbe

21. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb – Mjumbe
22. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb – Mjumbe
23. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb – Mjumbe
24. Mhe. Andrew John Chenge, Mb-Mjumbe Mwalikwa
25. Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb-Mjumbe Mwalikwa
26. Mhe. William Mganga Ngeleja, Mb-Mjumbe Mwalikwa
27. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka,Mb - Mjumbe Mwalikwa
28. Mhe. Ridhiwan Jakaya Kikwete, Mb - Mjumbe Mwalikwa

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashilillah kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Nd. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Nd. Angelina L. Sanga na Makatibu wa Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Nd. Dunford Mpelumbe, Nd. Stella Bwimbo, Nd. Chacha Nyakega, Nd. Angela Shekifu, Nd. Stanslaus Kagisa, Nd. Mkuta Masoli, Nd.Yona Kirumbi, na wasaidizi wao Nd.Grace Samuel na Nd. Gaitana Chima, kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA

24 JUNI, 2016